# INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION (IEBC)

IEBC
Your Vote, Your Future
INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION

# MWONGOZO RAHISI KWA USAJILI WA WAPIGA KURA KWA NJIA YA ELEKTRONIKI (BVR)



## Maswali yafuatayo yatakusaidia kuelewa shughuli ya kuwasajili wapiga kura:

### *1. Nini maana ya usajili wa wapiga kura?*
Usajili wa wapiga kura ni shughuli ya kunasa maelezo ya watu wanaofaa zikiwemo nambari za Kitambulisho cha Kitaifa ama Pasipoti katika sajili ama orodha ya wapiga kura

### *2. Nini sajili ya wapiga kura?*
Hii ni orodha ya watu waliosajiliwa na walio na haki ya kupiga kura. Ni wale tu majina yao yamejumuishwa katika sajili ya wapiga kura ambao wanaweza kushiriki uchaguzi ama kura ya maamuzi.

### *3. Nani atosha kusajiliwa kama mpiga kura?*
Ili kufaa kuwa mpiga kura, lazima uwe:
- Raia wa Kenya
- Miaka 18 na zaidi

### *4. Mbona kujisajili kama mpiga kura?*
Kujisajili kama mpiga kura kutakupa nafasi ya kuchagua viongozi wa taifa lako katika kiwango cha kitaifa na kaunti. Unaweza tu kushiriki uchaguzi iwapo umesajiliwa kama mpiga kura. Ni haki na wajibu wako kama raia anayewajibika kuchagua viongozi wako.

### *5. Nani huendesha shughuli ya usajili wa wapiga kura Kenya?*
Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) imepewa jukumu na Katiba pamoja na sheria zingine kutayarisha, kuhifadhi na kuhakiki sajili ya wapiga kura. Hufanya hivi kupitia maafisa wake wa usajili.

### *6. Afisa wa usajili ni nani?*
IEBC huajiri maafisa wa usajili kuendesha shughuli ya kuwasajili wapiga kura katika maeneo bunge. Maafisa wa usajili wanastahili:
a) Andika vyema majina ya wote wanaofaa katika sajili;
b) Ondoa majina ya wapiga kura waliofariki; na
c) Kufanya marekebisho yoyote rasmi yanayostahili kuhusiana na majina ya wapiga kura waliosajiliwa ama maelezo yoyote katika sajili ya wapiga kura.

### *7. Utajisajili wapi kama mpiga kura?*
Unaweza kujisajili kama mpiga kura katika kituo chochote cha usajili katika kaunti ama eneo bunge ambalo ungependa kupigia kura.

### *8. Ni wakati upi wa kujisajili kama mpiga kura?*
Kipindi cha kusajili wapiga kura kote nchini mara nyingi hutangazwa kabla ya uchaguzi mkuu ama kura ya maamuzi. Usajili utafanywa kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi na moja jioni kila siku ikiwemo wikendi. Vile vile, IEBC hufanya usajili wakati wote katika ofisi zake katika maeneo bunge, wakati wowote isipokuwa:
a) Katika kipindi mahususi kinachotangazwa na IEBC mara tu kabla ya tarehe ya uchaguzi mkuu;
b) Wakati wa uchaguzi mdogo, kati ya tarehe ya kutangazwa wazi kwa kiti cha eneo bunge husika na tarehe ya uchaguzi huo mdogo;
c) Katika hali ingine yoyote, kati ya tarehe ya kutangzwa wazi kwa kiti cha eneo bunge husika na tarehe ya uchaguzi.

### *9. Unajisajili vipi kama mpiga kura?*
Mtu lazima afike mwenyewe kwa afisa wa usajili ama makarani wa usajili walio chini yake katika kituo chochote cha usajili ili kuandikishwa kama mpiga kura.

### *10. Usajili unafanywaje?*
Usajili wa wapiga kura utafanywa kwa njia ya elektroniki, Biometric Voter Registration (BVR).

### *11. BVR ni nini?*
Biometric Voter Registration (BVR) ni njia ya kusajili wapiga kura kwa kutumia teknolojia ya kompyuta kunasa data za maumbile ya mtu kwa vile jina, umri, jinsia, alama za vidole na uso. Teknolojia hii inatumika kuthibitisha uhalisi wa wapiga kura na kuhakikisha uwazi na usadiki zaidi wa uchaguzi.

### *12. Je, vipi vifaa muhimu vya BVR?*
Vifaa vya BVR ni pamoja na:
a) Kompyuta ndogo ya mkononi (laptop)
b) Skena ya kuchukua alama za vidole
c) Kamera
d) Programu ya usajili
e) Hifadhi ya umeme (power back up source)
f) Pazia la nyuma la kuchukulia picha (Photo backdrop)

### *13. Nini inaifanya BVR bora zaidi katika kuunda sajili ya kuaminika?*
Habari za kibinafsi zinazonaswa na BVR ni za kipekee kwa kila mtu na haziwezi kutumiwa na mwingine. Hii inasaidia kuunda sajili ya kuaminika. BVR inahitaji kila mpiga kura kufika mwenyewe katika kituo cha kura ili kuhakikisha ni wapiga kura tu hakika ambao wamesajiliwa na wanaofika wenyewe siku ya uchaguzi ndio wanapiga kura.

### *14. Ni manufaa yapi ya BVR yaweza kulinganishwa dhidi ya sajili ya karatasi inayotumia mbinu ya Optical Mark Reader (OMR)?*
BVR ina manufaa yafuatayo dhidi ya mbinu za zamani za usajili;
a) Kipekee: BVR hunasa maelezo ya kipekee ya mtu. Ni vigumu kabisa kuwa na watu wawili walio na data sawia za maumbile.
b) Haiwezi kutumiwa na watu wawili: Data za maumbile zinazonaswa na BVR ni hususan za mtu binafsi na haziwezi kunakiliwa ama kuwa za watu wawili (huwezi kumpa mtu nakala ya uso ama vidole vyako!) hii haikuwa hivyo katika sajili ya awali ambapo nambari za vitambulisho ama pasipoti zilizotumika kumtambua mpiga kura zilikuwa rahisi kubuni ama kunakili.
c) Haiwezi kunakiliwa: Ni vigumu kabisa kubuni ama kudanganya maumbile. Hii inahakikisha maelezo yanayotolewa ni ya mtu aliye hai.
d) Haiwezi kupotea: Maumbile ya mtu yaweza tu kupotea katika ajali mbaya kabisa kinyume na sajili ya karatasi ambapo mpiga kura aweza kupoteza kadi yake ama kitambulisho na kikatumiwa na mlaghai kupigia kura.
e) Sahihu: BVR hunasa maelezo ya mpiga kura moja kwa moja katika kifaa cha teknolojia. Mpiga kura huthibitisha data hii kabla haijaakibishwa. Hii huchangia kuwepo kwa sajili sahihi nay a kuaminika.
f) Haraka: Mbinu hii hutoa fursa ya kunaasa maelezo kwa haraka na data hiyo haihitaji kuchambuliwa na kutengenezwa tena. Hii inakuwa haraka kuunganisha sajili ya wapiga kura kinyume na mbinu ya zamani iliyohitaji data kukaguliwa na kutengenezwa.
g) Epesi na sawasawa: BVR inahakikisha mpiga kura anatambulika kwa wepesi na sawasawa na ni msingi wa uchaguzi wowote wa kuaminika. Mbinu hii inatoa viwango vya juu kabisa vya usalama wa kupiga kura na inazuia udanganyifu katika uchaguzi.

### *15. Je, kuna mataifa mengine kando na Kenya ambayo yametumia BVR?*
NDIO! Mataifa haya ni Ghana, Nigeria, Gambia, DRC, Zambia, Sierra Leone, Namibia na Msumbiji.

### *16. Je, BVR ni salama?*
Mifumo ya kutambua na kuthibitisha data za maumbile zimetumika kwa zaidi ya miaka 25. Mbinu zinazotumika katika BVR hazina madhara yoyote ya kiafya.

### *17. Je, mahitaji yapi yafaa kutimizwa na mtu ili asajiliwe kwa kama mpiga kura kwa kutumia BVR?*
Kusajiliwa kama mpiga kura unahitaji kufika mwenyewe katika kituo cha usajili ukiandamana na stakabadhi zifuatazo za kujitambulisha;
a) Kitambulisho cha kitaifa ama
b) Pasipoti

### *18. Maelezo yapi yatanaswa na BVR?*
Habari zitakazonaswa na BVR ni pamoja na: jina la ukoo na majina mengine, tarehe ya kuzaliwa, umri, jinsia, alama za vidole, picha ya uso, na data za uchaguzi (eneo bunge, vituo vya usajili na kadhalika)

### *19. Je, mtu asiye na mikono aweza kusajiliwa kwa kutumia BVR?*
Iwapo hakuna mikono, BVR inatoa fursa kwa hali za kipekee ambapo wapiga kura walio na ulemavu wanaambatishwa ipasavyo na nyuso zao kutumiwa kuwasajili na kuwatambua.

### *20. BVR itaendeshwaje ?*
Watu wote wafaa kufika wenyewe katika vituo vilivyotengwa kwa usajili (yaani, vituo vya kawaida vya kupiga kura) ili kusajiliwa kama mpiga kura.
a) Usajili; awamu ya kujiandikisha. Data zifuatazo za maumbile zitanaswa: majina kamili ya anayesajiliwa, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, alama za vidole, picha, kituo cha uchaguzi (kituo cha kupiga kura, wodi ya kaunti, eneo bunge na kaunti), namabari za mawasiliano, hali ya usajili, nambari spesheli ya mpiga kura, aina ya stakabadhi ya kumtambua (kitambulisho cha kitaifa ama Pasipoti), na stakabadhi ya kumtambua.
b) Utengenezaji: Seva Kuu ya Maumbile (Central Biometric Server) inayotumia teknolojia ya kisasa ya kutambua alama za vidole, Automated Fingerprint Identification System (AFIS) itatengeneza rekodi za wapiga kura ili kutambua rekodi zilizonakiliwa. Rekodi hizi spesheli zitatengeneza sajili ya muda kwa kila kituo cha usajili/kupiga kura. Orodha maalum ya waliojisajili marudufu na kasoro zingine katika shughuli ya usajili kwa kila kituo cha usajili/kupiga kura pia itatayarishwa.
c) Sajili ya muda ya wapiga kura itachapishwa pamoja na orodha hiyo maalum ya kasoro zitapelekwa katika kibtuo cha usajili/kupiga kura ili kukaguliwa.

### *21. Je, wapiga kura waliosajiliwa watapewa kadi ya kura?*
La. Wapiga kura waliosajiliwa watapewa kijikaratasi cha kuonyesha wamesajiliwa. Karatasi hiyo itakuwa na maelezo ya mpiga kura.

### *22. Je, wapiga kura waliosajiliwa kwa kutumia BVR watatambuliwaje wakati wa uchaguzi? Nini kitakuwa tofauti na mbinu ya zamani ya kuwatambua wapiga kura kwa sajili ya karatasi?*
BVR sio mbinu ya kupiga kura lakini ni tceknolojia ya kumtambua mpiga kura. Mpiga kura atatambuliwa siku ya uchaguzi kwa kutumia sajili ya uchaguzi ya kielektroniki kwa kutumia data za kimaumbile zilizonaswa wakati wa usajili kabla yake kuruhusiwa kupiga kura. Hakutatolewa kadi za kupiga kura. Atakachohitaji mtu itakuwa kitambulisho chake cha kitaifa na alama za vidole ili kuruhusiwa kupiga kura. Pamoja na sajili ya uchaguzi ya kielektroniki, nakala iliyochapishwa ya sajili ya wapiga kura itakuwepo katika vituo vyote vya kupiga kura.

### *23. Je, wakati upi mtu atazuiwa kujisajili?*
a) Iwapo wewe ni mufilisi ambaye hajaachiliwa;
b) Iwapo umepatikana na makosa na mahakama ya uchaguzi ama umeripotiwa kufanya kosa la uchaguzi miaka mitano iliyopita kabla ya uchaguzi unaofanyika;
c) Iwapo unazuiliwa kisheria ama uko chini ya kifungo cha kisheria;
d) Iwapo mahakama itakutangaza kama aliye na akili punguani.

### *24. Je, usajili endelezi unahusu nini?*
Unahusu kuendelea kuongeza majina ya watu na maelezo husika yanayohitajika kwa:
a) Waliohitimu kusajiliwa kama wapiga kura;
b) Wapiga kura waliosajiliwa ambao wangependa kuhamisha kura yao hadi maeneo ambayo wangependa kupigia kura;
c) Kuondoa kutoka kwa sajili majina ya wale waliofariki;
d) Kutambua wapiga kura waliojisajili mara mbili/kadha;
e) Kubadilisha maelezo ya usajili, kwa mfano, kubadilisha majina baada ya kuoa/kuolewa;
f) Kurekebisha makosa, kwa mfano, majina yaliyoandikwa visivyo, nambari za kitambulisho ama pasipoti zilizonakiliwa visivyo.

### *25. Je, sajili ya wapiga kura inasahihishwaje?*
Sajili ya wapiga kura inafanywa sahihi wakati afisa wa usajili:
a) Anaweka kwa usahihi maelezo ya waliohitimu katika sajili ya wapiga kura;
b) Anaondoa majina ya wapiga kura

**Endelea ukurasa unaofwata**

A NI

# INDEPENDENT ELECTORAL AND BOUNDARIES COMMISSION (IEBC)

## MWONGOZO RAHISI KWA USAJILI WA WAPIGA KURA KWA NJIA YA ELEKTRONIKI (BVR)



**Kutoka Ukurasa 1**

waliofariki kutoka kwa sajili;

c) Anaondoa kutoka kcwa sajili majina ya wale waliojiandikisha zaidi ya mara moja; na

d) Anaondoa majina ya wale ambao hawahitimu tena kusajiliwa kama wapiga kura.

### 26. Je, ni upi wajibu wa mpiga kura kuhakikisha sajili ni sahihi?

Ni jukumu la kila mpiga kura aliyesajiliwa kukagua sajili na kufahamisha maafisa wa usajili kuhusu marekebisho yoyote wangependa kufanya kuhusu maelezo yao katika sajili ya wapiga kura.

### 27. Je, ukaguzi wa sajili ya wapiga kura ni nini?

Hii ni shughuli ambapo wapiga kura huchambua sajili ili kuhakikisha kwamba;

a) Ni wale waliohitimu pekee wamesajiliwa;

b) Majina na maelezo ya waliohitimu yamenaswa vyema katika sajili;

c) Majina yao yameandikwa vizuri;

d) Nambari ya kitambulisho cha kitaifa ama pasipoti imeandikwa vizuri;

e) Majina ya waliofariki hayapo kwenye sajili ya wapiga kura;

f) Wapiga kuwa waliojisajili mara mbili/kadha hawapo katika sajili.

### 28. Je, mpiga kura aliyesajiliwa anaruhusiwa kujisajili mara zaidi ya moja kama mpiga kura?

LA! Mtu anaruhusiwa kujisajili mara moja btu kaika eneo bunge ama kituo cha usajili cha chaguo lake. Sheria inasema ni makosa kujisajili zaidi ya mara moja kama mpiga kura katika vituo ama eneo bunge zaidi ya moja.

### 29. Ni adhabu ipi inatolewa kwa kujisajili zaidi ya mara moja?

Ni kosa kubwa kujisajili zaidi ya mara moja. Watu waliojisajili zaidi ya mara moja kama wapiga kura wakipatikana na makosa watapigwa faini isiyozidi shilingi elfu mia moja ama kutupwa jela kwa muda usiozidi mwaka mmoja ama kupewa adhabu zote mbili. Watu hawa watazuiwa kushiriki uchaguzi mkuu unaofuata karibuni na ujao. Ni bora na busara kutokujisajili zaidi ya mara moja.

### 30. Je, nini makosa ya uchaguzi wakati wa usajili wa wapiga kura?

Vitendo hivi ni vile vinakiuka kanuni na masharti ya usajili. kosa hufanyika pale mtu hujisajili kama mpiga kura katika kituo zaidi ya moja cha usajili. makosa mengine yanayoweza kutendwa wakati wa shughuli ya usajili wa wapigaa kura nji pamoja na:

a) Kutoa kimakusudi maelezo ya uongo juu ya ama kuhusiana na data yoyote itakayonaswa katika sajili yoyyote ya wapiga kura; ama

b) Bila ruhusa kutengeneza, kutayarisha, ama kuchapisha stakabadhi ama karatasi inayofanana ama inayokusudia kuwa sajili ya wapiga kura; ama

c) Kusaidia, kushiriki, kushauri ama kuwezesha kutokea kwa ama jaribio la kufanya makosa yoyote yaliyotajwa hapa juu.

### 31. Je, adhabu zipi zitatolewa kwa makosa haya?

Mtu yeyote anayefanya makosa haya akipatikana na hatia atapigwa faini isiyozidi shilingi milioni moja ama kufungwa jela kwa muda usiozidi miaka sita ama kupewa adhabu zote.


### 32. Je, mtu aweza kuhamia kama mpiga kura kwa kituo kingine cha usajili ama eneo bunge?

NDIO! Mtu aweza kuhamia kama mpiga kura kwa kituo kingine cha usajili katika eneo bunge lake ama nje ya eneo bunge lake. Mtu huyo anahitajika kufika mwenyewe katika kituo hicho cha usajili ama eneo bunge hilo analotaaka kuhamia iwapo anatimiza mahitaji.

### 33. Je, twawezaje kueneza ujumbe kuhusu habari za usajili wa wapiga kura?

Wakenya wote wenye nia njema, viongozi wa kijamii, viongozi wa kidini, machifu na manaibu wa chifu wanaombwa kusaidia kueneza habari kuhusu usajili wa wapiga kura katika maeneo yao. Hii itasaidia Wakenya zaidi kujisajili kama wapiga kura, na hivyo kushiriki vilivyo katika kuwachagua viongozi wao. Mpiga kura aliye na ufahamu hufanya uamuzi wa busara. Kumbuka, utafanya hivi tu iwapo wewe ni mpiga kura uliyesajiliwa.

## USAJILI WA WAPIGA KURA KWA NJIA YAELEKTRONIKI (BVR) NI NYEPESI, YAVUTIA NA RAHISI KUFUATA KAMA INAVYOELEZWA HAPA CHINI:




**Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na makao makuu ya IEBC, jumba la Anniversary Towers, Orofa 6, barabara ya University Way, Nairobi.** Simu: +254 (020) 2769000, barua pepe: info@iebc.or.ke, www.iebc.or.ke

**AU**

**Ofisi ya IEBC ya Eneo**

**AU**

**Ofisi ya Eneo Bunge iliyo karibu**

***Your Vote, Your Future***